

- chote cha matibabu
- Usikatishe dozi unapojisikia nafuu
 - Ni muhimu kumaliza dozi ya dawa zote ulizopewa
 - Usimpe mgonjwa mwingine dawa zako
 - Kumbuka kutumia dawa kwa uangalifu na kufuata masharti ulizopewa

“Ongea na daktari au mfamasia ili kupata maelezo sahihi ya ugonjwa unaokusumbua na dawa ulizopewa”

‘Una haki ya kujua dawa ulizopewa zinatibu nini na zinatumiwaje’



Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),
S.L.P 1253 Dodoma au 77150 Dar es salaam.

Simu+255 22 2450512/2450751/2452108

Barua pepe: info@tmda.go.tz

Tovuti: www.tmda.go.tz

Simu bila malipo: 0800110084



@tmdatanzania

Kanda ya Ziwa

Barabara ya Nyasaka,

Nyakato Buzuruga,

S.L.P 543,

Ilemela - Mwanza

Simu +255 28 2981224/5

Barua pepe: info.mwanza@tmda.go.tz

Kanda ya Kaskazini

Eneo la Sakina.

S.L.P 16609, Arusha

Simu +255 272970333/737782442

Barua pepe: info.arusha@tmda.go.tz

Kanda ya Mashariki

Jengo la GEPPF,

Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,

S.L.P 31356,

Dar es salaam,

Simu +255 739 226328/788470312

Barua pepe: info.easternzone@tmda.go.tz

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

Jengo NHIF ghorofa ya 3.

S.L.P 6171, Mbeya

Simu +255 252504425

Barua pepe: info.mbeya@tmda.go.tz

Kanda ya Kati

S.L.P 1253 Dodoma.

Simu +255 26 2320156

Barua pepe: info.dodoma@tmda.go.tz

Kanda ya Kusini

Jengo la PSSSF,

S.L.P 1447, Mtwara.

Simu: +255 232334655

Barua pepe: info.mtwara@tmda.go.tz

Kanda ya Magharibi

Jengo la TUWASA,

S.L.P 520, Tabora

Simu +255 262606082

Barua pepe: info.tabora@tmda.go.tz

TMDA - Hulinda Afya ya Jamii

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA

Tanzania Medicines & Medical Device Authority

**MATUMIZI SAHIHI
YA DAWA:
VIJIUASUMU
(ANTIBIOTICS)**



Utangulizi

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Vijiwasumu (antibiotics) ni mojawapo ya dawa muhimu katika kutibu magonjwa mbalimbali hasa yatokanayo na vijimelea vya maradhi. Zikitumiwa ipasavyo dawa hizi huweza kuokoa maisha, lakini matumizi mabaya huleta madhara kwa mtumiaji. Mfano wa dawa ni Ampicillin, Ciprofloxacin, Tetracycline, PPF, Gentamycin, Pen V, Erythromycin, Metronidazole nk.

Vijiwasumu huua bakteria, baadhi ya bakteria huweza kujenga usugu dhidi ya dawa hizi. Ugonjwa unaotokana na bakteria hawa unakua mgumu kutibika na unaweza kuambukizwa kwa watu wengine. Ili kutibu ugonjwa unaotokana na bakteria sugu unahitaji dawa yenye nguvu zaidi na wakati mwingine inabidi mgonjwa kulazwa hospitalini kwa uangalizi na matibabu zaidi.

“Kutumia vijiwasumu kiholela huweza kusababisha usugu wa bakteria na hivyo kushindwa kufanya kazi ipasavyo”

Kwa namna gani bakteria huwa sugu?

Kila wakati unapotumia vijiwasumu, bakteria wasio sugu hufa na kubaki walio sugu. Matumizi ya mara kwa mara na holela ya vijiwasumu husababisha bakteria kuwa sugu. Bacteria hawa huweza kusambaa katika familia na jamii nzima kwa ujumla



EPUKA

Epuka matumizi yasiyosahihi ya vijiwasumu. Baadhi yetu hatutumii dawa kwa kufuata maelezo tuliyopewa na wataalamu bali tunazitumia kiholela. Hii ni hatari kwa maisha yetu.

“Ni muhimu kufuata maelekezo uliyopewa na daktari au mfamasia. Usitumia dawa kiholela”

Matumizi yasiyosahihi ya vijiwasumu ni yapi?

- Kununua kiholela na kutumia dawa bila kufanyiwa uchunguzi au kuelekezwa na daktari
- Kutumia vijiwasumu kutibu magonjwa yanayotokana na virusi (viral infections)
- Kutumia dozi isiyosahihi
- Kushindwa kumaliza dozi
- Kutumia dawa zinazolingiliana kiutendaji kwa pamoja, kwa mfano Tetracycline na Magnesium
- Kutumia dawa na pombe

“Vijiwasumu vinapotumiwa kwa uangalifu, vinaweza kuokoa maisha”

USHAURI

Ili kuepuka au kupunguza kutokea usugu wa bakteria unashauriwa kutumia dawa kwa usahihi

- Usinunue vijiwasumu kiholela
- Usinunue vijiwasumu bila cheti cha daktari
- Hakikisha unafhamu matumizi sahihi ya dawa ulizopewa kabla ya kurudi nyumbani toka kituo cha afya au duka la dawa
- Tumia dozi sahihi kwa kipindi